



# KAREMA YETU



Vol.1. ISSUE NO. 28

Monday 6<sup>th</sup> February 2017

Your Local Voice!

## KATIKA WIKI HII.....

- **MATOKEO KIDATO CHA NNE:**
  - Wasichana wavunja rekodi kwa kupindua historia ya Shule.
  - Ufaulu wao waamsha matumaini mapya.
- **UJENZI WA BWENI WASHIKA KASI:**
  - Matumaini mapya yaanza kuonekana.
- **MICHEZO NA BURUDANI:**
  - Kidato cha Pili 'Hakunaga'.
  - Wawaliza kaka zao.
  - Kidato cha Tatu akili za wayumba.

## KUTOKA MEZA YA MHARIRI:

### Siri ya Mafanikio ya Kidato cha Nne 2016:

Unapotaja 'Siri ya Mafanikio' kila mtu ana siri yake ya mafanikio katika kila jambo analofanya. Wataalam wa Soka, kwa mfano, wanaamini kuwa siri ya mafanikio ya mchezaji yeyote ni kujituma kwenye mazoezi, la sivyo hawezi kufanikiwa.

Hata tukija katika suala la kusoma, siri ya kufaulu ni kujituma kusoma. Kujituma na nidhamu ndio siri ya mafanikio ya wanafunzi wengi.

*"Form Four 2016 worked hard for their part; you have to work hard for your part too".*

Kaa bure uletewe mabaki, tembea upate kile unachokipenda.

Congratulations Form Four 2016!

## QUOTE OF THE DAY:

"You can give your best and think BIG"  
-Ben Carson.

## MATOKEO YA KIDATO CHA NNE; Wasichana Wapindua...

### Na Emmy Benny

Matokeo ya kidato cha nne 2016 yaliyotoka tarehe 31/01/2017 yamerudisha matumaini ya wengi hasa baada ya Shule ya Sekondari Karema kufanya vizuri kwa kushika nafasi ya kwanza kiwilaya, na wasichana wakivuja rekodi kwa kufanya vizuri na kufaulu kwa wingi tofauti na miaka ya nyuma tangu kuanzishwa kwa shule hii.

Kwa mara ya kwanza Karema Sekondari imetoa wasichana 6 kwa ufaulu wa daraja la 3, hivyo kuamsha matumaini mapya ya ufaulu kwa upande wa wasichana. Wanafunzi waliofanya mtihani walikuwa 58 na waliofaulu ni 48 kuanzia daraja la 2 hadi la 4 huku wanafunzi 10 wakifeli.

Mhariri pamoja na Waandishi wa gazeti pendwa la **KAREMA YETU** wanatoa pongezi kwa uongozi mzima wa shule, walimu, wazazi, walezi, wanafunzi wa kidato cha nne 2016, na wanafunzi wote wa Karema Sekondari kwa ujumla.

## UJENZI WA BWENI.....

### Na Hellen Cruz

Hali ya bwani jipya imeanza kuonesha matumaini baada ya mafundi kuonekana wakifanya kazi kwa nguvu ili kumaliza haraka. Muda wote wameonekana wakiwa 'busy' kitu kinachotia moyo huku wanafunzi wakisali kimy kimya bwani liishe 'fasta' ili foleni ipungue.



# KAREMA YETU



Vol.1. ISSUE NO. 28

Monday 6<sup>th</sup> February 2017

Your Local Voice!

Ahadi za viongozi zinaonekana kutimia na mafanikio kuonekana. Wanafunzii eeh! Utaipendaaa.....!

## MICHEZO NA BURUDANI

Na Emmy Benny

“Haina kudevela.....!!”

Limeoneshwa na timu ya mpira wa miguu ya kidato cha Pili kwa kuwalisha magoli ya maana kaka zao wa kidato cha Tatu. Licha ya mvua kubwa kunyesha tangu alfajiri mpaka saa 5 asubuhi na kusababisha uwanja kujaa maji, lakini kidato cha Pili hawakuona kama hilo ni tatizo kwao, kwani walidhamiria kuwatia adabu kaka zao na hali ilikuwa hivyo.

Kama Waswahili wasemavyo “Mtoto akililia wembe mpe”, kidato cha Pili walitoa dozi hiyo ya mabao 3-1 dhidi ya kidato cha Tatu waliolilia mechi hiyo kabla. Pamoja na ubabe wote wa kidato cha Tatu, mpaka mechi inamalizika, kidato cha Pili ndio walioibuka washindi na kutwaa ubabe wa siku hiyo.



© Copyright. KaremYetu 2017